

## Athari za Ulumbilugha Mionganoni mwa Chokoraa

Ruth M. Binyanya<sup>1</sup>, Ayub Mukhwana<sup>1</sup> na Samuel M. Obuchi<sup>2</sup>

<sup>1</sup>Chuo Kikuu cha Nairobi

<sup>2</sup>Chuo Kikuu cha Moi

### Ikisiri

Makala haya yanachunguza athari za ulumbilugha katika kutimiza nia za wakati husika za Chokoraa. Chokoraa hutumia lugha mbalimbali katika mawasiliano yao. Uteuzi wa lugha itakayotumiwa na Chokoraa hutegemea muktadha maalum. Chokoraa hutumia Kiswahili, Sheng', Kiingereza na lugha za asili katika mazungumzo yao. Ulumbilugha ndio huwafanya Chokoraa wakati mwingine kuchanganya ndimi kwa kutumia lugha ambazo wanazijua huku wakitaka kutimiza nia mahsus. Kwa hali hii basi tunaweza kusema kuwa wanaulumbilugha huteua lugha kwa mujibu wa muktadha kutoptera na ukweli kuwa lugha moja yaweza kuwa faafu katika muktadha mmoja na wala sio mwingine. Pia, makala haya yanaainisha athari za ulumbilugha kama zinavyojitokeza katika mazungumzo ya Chokoraa wa mtaa duni wa Mathare, jijini Nairobi.

**Maneno Muhimu:** ulumbilugha, lugha mkakati, chokoraa

### Utangulizi na Mapitio ya Maandishi

Lugha hutumiwa na wanajamii kufanikisha mawasiliano yao. Makundi mbalimbali ya kijamii hutumia lugha kwa namna ya kipekee. Upekee huu wa matumizi ya lugha ndio hutumiwa kutambulisha kundi husika kwa misingi ya lugha. Jamii yenye ulumbilugha hutumia lugha wazijuazo kwa kuzibadilisha ili kukidhi haja ya mawasiliano yao na hili ni jambo ambalo hutokeea pia kwa Chokoraa. Watu huchanganya ndimi kwa sababu mbalimbali kukiwemo kufidia msamiati au kujieleza ipasavyo. Hali hii inaonyesha kuwa lugha fulani huweza kupungukiwa kimsamiati au mzungumzaji anawezakosa kufahamu msamiati husika na hivyo basi kutumia maneno ya lugha nyingine katika mazungumzo yake. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa uchanganyaji lugha hauwezi kuuepukika kwa jamii yenye ulumbilugha. Tuligundua kuwa Chokoraa huathiriwa na ulumbilugha kiasi cha kuwafanya kuchanganya ndimi katika mazungumzo yao na kuunda maneno ya Sheng' kutoptera na Kiswahili na Kiingereza.

Dhana ulumbilugha ni kisawe cha wingilugha. Dhana hii imeangaziwa na wasomi kama vile Iribemwangi na Mukhwana (2011) ambao wanasesha kuwa wingilugha ni hali ya jamii kuwa na ujuzi wa lugha nyingi na ambazo wanawea kuzitumia katika mawasiliano yao. Habwe na wenzake (2010) wanauona

wingilugha kama uwezo wa jamii kutumia lugha zaidi ya mbili katika mawasiliano. Wasomi hawa wanaafikiana kuwa ulumbilugha ni uwezo wa mtu au jamii kutumia lugha mbalimbali katika mawasiliano yake. Maoni ya wasomi hawa yanaelekeea kuwa sawa kwa kuwa wote wanakubaliana kuwa ulumbilugha unahu su matumizi ya lugha zaidi ya moja katika mazungumzo. Kwa upande wetu, tunauona ulumbilugha kama ujuzi wa kutumia lugha kadhaa kwa kuzibadilisha katika mazungumzo ili kukidhi mahitaji ya kimawasiliano ya wakati husika. Katika makala haya, tutajikita kwa maoni ya Massamba (2004) ambaye anasema kuwa ulumbilugha ni uwezo wa kutumia lugha mbili au zaidi katika mazungumzo yake. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa wanawingi lugha hutumia lugha kwa kuzibadilisha katika mawasiliano yao. Matumizi ya lugha fulani huchochewa na hali za wazungumzaji, muktadha wa mazungumzo na nia zao za wakati husika.

*Chokoraa* ni kikundi cha kijamii cha kipekee kwa namna wanavyotumia lugha. Watafiti Lewis (2012), Flowers (2010), Shorter na Onyancha (1999), na Suda (1997) wanasema kuwa *Chokoraa* ni watu ambao hawana mahali wanapopaita nyumbani ila mitaani. Watu hawa hulala na kuendeleza shughuli zao zote mitaani. Maisha ya mitaani huwafanya *Chokoraa* kuzungumza na watu wengine kwa nia ya kupata kazi kama vile ya kubeba mizigo. Mahusiano mionganoni mwa *Chokoraa* na pia baina ya *Chokoraa* na watu wengine hudhihirisha matumizi mbalimbali ya lugha ambayo husababisha uchanganyaji lugha.

Jamii huchagua lugha ipi itumike wapi na vipi. Jambo hili huathiri matumizi ya lugha ya jamii ili kutosheleza mahitaji yao ya wakati husika. Mazingira na hali za watu ni mojawapo wa viamu zi vya matumizi ya lugha. *Chokoraa* hujipata katika hali mbalimbali. Hali hizi huwafanya kuteua lugha tumizi ili waweze kufanikisha mawasiliano yao na kutimiza nia zao za wakati husika. Lugha ya *Chokoraa* huchochewa zaidi na shughuli wanazozitekeleza. *Chokoraa* hupata riziki yao kwa kuokota viliviyotupwa, uchuuzi, na pia kuwaibia watu. Wakati mwininge, *Chokoraa* hufanya kazi kama vile kuosha magari na kuwabebea wafanyibiashara mizigo. Kazi hizi huzua uchanganyaji lugha. Kandagor (2000), Ogechi na Jwan (2004) wanasema kuwa *Chokoraa* hutumia Sheng', Kiswahili na lugha nyininge za kwanza katika mazungumzo yao. Matumizi haya ya lugha zaidi ya mbili katika mawasiliano hutokana na ulumbilugha katika jamii husika.

Matumizi ya lugha ya mtu hutegemea tajriba yake ya maisha (Leech na Short, 1981). *Chokoraa* huishi barabarani. Watu huwabeza na wao hufukuzwa na polisi au askari wa kaunti. Hali hii huathiri matumizi yao ya lugha. Lugha inayotumiwa na kikundi fulani cha kijamii ni chombo cha kujieleza na kujitambulisha na kikundi hicho. Lugha ya *Chokoraa* hubadilikabadilika kutegemea hali zinazowakumba na pia kama wanawasiliana na nani. *Chokoraa* wanapokuwa mitaani, huunda familia zao za kupanga. Familia hizi za kupanga huweza kuhusisha familia asilia ya baba, mama na watoto au watu kutoka sehemu

---

mbalimbali ila wakaungana na kuunda familia. Familia hizi huishi katika eneo moja na husaidiana kwa hali na mali. Ripoti iliyotolewa na NCBDA, Julai, 2001, inaonyesha kuwa familia za barabarani huwa na sifa zifuatazo: umoja, ushirikiano katika shughuli zao zote na huishi katika eneo fulani ambalo linajulikana kama kwao. NCBDA wanaonyesha pia kuwa *Chokoraa* katika familia hizi huwa na misimbo yao iliyo tofauti na ya familia zingine. Lugha yao ndiyo kitambulisho chao na ndiyo huwawezesha kutekeleza shughuli zao za kila siku. Lugha ya *Chokoraa* ni lugha ambayo huwawezesha kutimiza haja zao za kimawasiliano za wakati husika.

Uchaguzi wa aina ya lugha itakayotumiwa na kikundi fulani ni zao la hali tofauti tofauti. Maana ya usemi fulani itajidhihirisha wazi kutegemea muktadha husika. Kwa mujibu wa Leech (1969) kichocheo kikuu cha uchanganyaji lugha ni hali ambayo humkumba mzungumzaji. Anaeleza kuwa ni kawaida kuainisha hali ambazo hukumba uteuzi na utumizi wa lugha kwa kuchunguza nyenzo ya uwasilishaji, uhusiano wa washiriki na nia ya mazungumzo hayo. Namna *Chokoraa* huzungumza huchochewa na hali zinazowakumba. Uhusiano wao umejengeka kwa kujipata katika hali sawa. Shirika la CSC lasema kuwa hali yao ya kuwa wamekata tamaa ya maisha mema huchangia tabia zao. Tabia ambazo zinahusisha kutumia lugha inayoeleweka na washiriki wote wa mazungumzo hayo na ya upole wanapotaka kusaidiwa na kuwa wakali ikiwa wanataka kitu kwa lazima.

### Mkabala wa Kinadharia

Matumizi ya lugha ya kundi la kijamii la *Chokoraa* yamejadiliwa na kufafanuliwa na wataalamu mbalimbali wakiwemo Githiora (2002), Abdulaziz na Osinde (1997) Suda (1994, 1997) na Ray (2017). Kila mmoja kati ya wataalamu hawa ametumia nadharia yake kulingana na lengo la utafiti wake. Wasomi hawa wanasema kuwa *Chokoraa* wa Kenya hutumia Sheng' katika mazungumzo yao ila sisi tunasema kuwa *Chokoraa* hawa hutumia lugha zaidi ya moja katika mazungumzo yao kutohana na athari ya ulumbilugha na kuwa wao hutumia lugha itakayoafiki muktadha husika. Katika makala haya, nadharia ya kumudu imetumika ili kufafanua athari za ulumbilugha katika mazungumzo ya *Chokoraa* wa Mathare.

Nadharia hii iliasisiwa na Gibson (baina ya 1977 na 1986) na ikakuzwa na wasomi kama vile Aronin na Singleton (2007, 2010 na 2012). Aronin na Singleton walifuata mkabala wa isimujamii katika kueleza mihimili ya nadharia hii ya kumudu wakati ambapo Gibson (1977) alijikita kwa wanyama kwa kutaka kujua uhusiano uliopo baina ya wanyama na mazingira yao na namna mazingira hayo huathiri tabia zao na katika mwaka wa 1986, Gibson alishughulikia namna watu hutumia lugha kwa mujibu wa mazingira yao. Katika utafiti wake, Gibson aligundua kuwa mtu hawezi kutenganisha lugha na mazingira. Hii ni kwa sababu wanaulumbilugha hutumia lugha mbalimbali katika mazingira mbalimbali ili kuafiki nia zao za wakati husika. Kwa upande mwingine, Aronin na Singleton

(2007) walichunguza madai ya Gibson kuhusu nadharia ya kumudu kwa mkabala wa isimujamii na wakagundua kuwa wanaulumbilugha huteua lugha ya kutumia katika muktadha fulani kwa kuzingatia uwezekano na umuhimu wa kutumia lugha fulani katika muktadha fulani.

Wataalamu hawa wanakubaliana kuwa kumudu kwa lugha huambatana na tabia za watu. Hali hii huwawezesha wanaulumbilugha kumudu lugha wazijuazo huku wakidhihirisha upekee wao na hili ni jambo ambalo linaweza kutumiwa kuwatambulisha *Chokoraa* kama kikundi mahsusii cha kijamii. Hali ya kumudu lugha mbalimbali hutofautiana kutoka kwa mtu mmoja hadi mwengine. Aronin na Singleton (2012) waliangazia tena nadharia hii ya kumudu na wakashughulikia aina mbalimbali za kumudu lugha ambapo walishughulikia kategoria mbili ambazo ni: umudu lugha wa jamii na ule wa kibinafsi. Waligundua kuwa umudu lugha wa kijamii huathiri umudu lugha wa kibinafsi. Hii ni kwa sababu umudu lugha wa kijamii huhusisha lugha ambazo hutumiwa jamii husika. Umudu lugha wa kijamii huchochewa na hali mbalimbali za kijamii kukiwemo tabaka na malezi, kazi wazifanyazo, kiwango chao cha elimu. Kwa upande mwengine, wasomi hawa wanauona umudu lugha wa kibinafsi kama matumizi ya lugha ya mtu binafsi hata ingawa mtu huyo hutumia lugha kutegemea na mazingira alimokulia na vile vile nia ya mazungumzo yake ya wakati huo husika.

Nadharia ya kumudu ilituwezesha kufafanua athari za ulumbilugha katika mazungumzo ya *Chokoraa* hasa katika kutimiza nia zao na kuwawezesha kupambana na changamoto wazipitiao mitaani. Kwa mujibu wa nadharia ya kumudu mazingira na hali za watu huwafanya wanaulumbilugha kutumia lugha mwafaka ili kutimiza malengo ya mazungumzo hayo. Nia za *Chokoraa* za wakati husika huwafanya aidha kutumia lugha itakayoeleweka na kila mshiriki wa mazungumzo hayo au lugha ambayo itaficha siri zao. Vile vile, *Chokoraa* wanaweza kuchanganya ndimi katika mazungumzo yao huku wakitumia lugha zao za kwanza, Kiswahili, Kiingereza na Sheng' kutegemea nia ya mazungumzo husika.

### Mbinu za Utafiti

Data ambayo imetumiwa katika makala haya ilikusanywa na Ruth baina ya Januari-Agosti, 2020 katika maeneo mbalimbali ya mtaa wa mabanda wa Mathare, jijini Nairobi ambapo alijikita kwa matumizi ya lugha kimkakati katika kutimiza nia mbalimbali za wanafamilia wa mitaani, kwa ajili ya tasnifu yake ya Uzamifu. Data hiyo inatumika katika makala haya kwa nia ya kuonyesha namna ulumbilugha huathiri matumizi ya lugha ya *Chokoraa* kwa nia ya kutimiza mahitaji mbalimbali ya kimawasiliano. Data yenye ilikusanywa kwa kutumia sampuli ya uongezeaji-kadri. Kwa mujibu wa Christopoulos (2010) na shirika la Social Research Update (2017) sampuli ya uongezeaji-kadri ni ile hali ya kukusanya data kwa kuchagua mtu mmoja kutoka kwa walengwa wa utafiti kisha mtu huyo anamuongoza mtafiti kwa mtu mwengine wa kundi husika. Sampuli hii

ya uongezeaji-kadri ilikuwa mwafaka kwa kuwa *Chokoraa* wa Mathare wamejipanga katika makundi ya kifamilia na kwa hali hii familia moja ya kupanga ilitutambulisha kwa familia nyine ya mitaani mtaani Mathare, Nairobi. Sampuli ya uongezeaji-kadri ilituwezesha kupata data kutoka kwa watu tofauti wa kikundi cha kijamii cha *Chokoraa* wa Mathare na kwa wakati tofauti. Vile vile, data ilikusanya kupitia uchunguzi shiriki ambapo mtafiti hakujitambulisha kwa *Chokoraa* kuwa alikuwa anafanya utafiti jambo ambalo lilimwezesha kupata data katika uasilia wake. Mtafiti aliona na kushuhudia namna *Chokoraa* wa Mathare, jijini Nairobi hutumia lugha mbalimbali kutokana na kuathiriwa na ulumbilugha ili kutimiza nia zao za wakati husika kukiwemo kuomba kazi au hata pesa kutoka kwa watu wengine wa makundi-nje.

Mtafiti aliwasiliana na *Chokoraa* wa Mathare ana kwa ana kwa kutumia maswali yasiyo ya moja kwa moja na ambayo yalimwezesha kupata data faafu ili kuelezea athari za ulumbilugha katika mawasiliano yao. Mbinu tatu zilitumiwa katika kukusanya data husika: kurekodi, mazungumzo ya ana kwa ana na kushuhudia. Tulirekodi mazungumzo ya utafiti kwa kutumia kinasa sauti cha kidijitali ambacho kilikuwa mfukoni mwa mtafiti. Kinasa-sauti cha kidijitali kilitumiwa kwa sababu ya hali ya kiteknolojia inayobadilika kila uchao, ni rahisi kukibeba, na kiliweza kuhifadhi data kwa matumizi ya baadaye. Data yenewe ilisikilizwa, ikaandikwa na kisha kuchanganuliwa kwa njia ya kinathari. Mtindo wa uchanganuzi data kinathari hujikita zaidi kwa muktadha wa mazungumzo na ndio maana umetumika katika makala haya. *Chokoraa* walilotumika katika utafiti huu walirejelewa kwa kutumi nambari (yaani mtu 1, mtu 2, na kuendelea) katika kila mazungumzo huku washiriki wengine wa mazungumzo hayo wakirejelewa kwa kazi wanazofanya kama vile mtafiti kisha data ilichanganuliwa kwa mujibu wa nadharia ya Kumudu.

#### Athari za Ulumbilugha Katika Mazungumzo ya *Chokoraa*

*Chokoraa* wa Mathare jijini Nairobi ni watu kutoka jamiilugha mbalimbali na ambao wanaweza kutambuliwa kwa misingi ya matumizi yao ya lugha. Tulibaini kuwa *Chokoraa* wa Mathare ni wanaulumbilugha kutokana na matumizi yao ya Kiswahili, Kiingereza, lugha za kiasili na Sheng' katika mazungumzo yao. *Chokoraa* hawa wanaweza kuwasiliana kwa kutumia Kiswahili pekee katika mazungumzo yao hasa wanapozungumza na wanakundi-nje kama vile wapiti njia. Matumizi ya lugha ya Kiswahili huwa mwafaka kwa *Chokoraa* wanapoomba msaada kutoka kwa wapita njia wasiowafahamu. Hii ni kwa sababu Kiswahili ni lugha sambazi jijini Nairobi kama asemavyo Githiora (2002). *Chokoraa* wa Mathare vile vile wanaweza kuwasiliana kwa kuchanganya ndimi katika mawasiliano yao hasa wanapokuwa wakizungumza wenyewe kwa wenyewe.

### Uchanganyaji ndimi

Athari kuu ya ulumbilugha ni uchanganyaji ndimi katika mawasiliano kiasi cha kutumia lugha zaidi ya mbili katika mazungumzo kama inavyobainika katika diskosi ifuatayo:

1. Mtu 1: **Haki ile vitu tunafanyianga hawa wamama better (afadhali) ukae single (kapera) Kuliko kusumbua msichana wa mtu.**

Mtu 3: **Ukae tu bure, aje sasa,**

Mtu 2: **Wee acha chocha.**

Mtu 1: **Si chocha brathe (ndugu), usikie stori yangu utakubaliana na mimi tu.**

Mtu 4: **Kwani wewe ni mumama?**

Mtu 1: **Sio hivyo, but (ila) ile maisha mokoro (mamangu) wangu alikuwa anapitia nikiona, ndio ilinifanya niko hapa haki, saa hii ningekuwa nimemaliza mesty (shule) na..**

Mtu 3: **Leta hiyo riba (hadithi) jooh tuone ka inamatch (fanana) na yetu.**

Mtu 1: **Mzae (baba) alikuwa akiingia tu hivi kila kitu inachange (inabadilika) manze, anataka apewe nyake (nyama) na ugali na hata hataki kujua itatoka wapi, akikosa anaanza kumpea beating tukiwa tumeketi tunawawatch (tazama) tu. Mathee (mama) hadi anafaint (zirai) na...**

Mtu 4: **Mimi nilikuwa namshika mashati akijaribu kumchapa mokoro (mama) wangu, aai singeentertain ku...**

Mtu 2: **Sa unafight (pigana) na buda (baba) yako?**

Mtu 4: **Weee unajua tuliwatch (tazama) akipiga tu mokoro (mama) tangu tukiwa watoi, na bado akaendelea tu, nilifika class (darasa) seven (saba) nikaamua kama mbaya, mbaya, akimchapa na mi nampiga hata na mwiko, hadi nilitoka kwake hivyo, sipendangi ujinga mimi.**

Haya ni mazungumzo mionganoni mwa *Chokoraa* wa jinsia ya kiume mtaani Mathare, katika eneo la Kosovo 3A. Katika mazungumzo haya, *Chokoraa* hawa wanenye wametumia Kiswahili, Sheng' na Kiingereza, kwa mfano, Mtu 1 katika kipengele cha 3 ametumia Kiswahili na Kiingereza, anasema "**haki ile vitu tunafanyianga hawa wamama better ukae single kuliko kusumbua msichana wa mtu.**" Katika usemi huu, maneno *better* na *single* ni ya Kiingereza kwa maana ya afadhali na mseja mtawalia. Kiswahili kimetawala katika usemi huu licha ya kuwa Mtu 1 anachopeka maneno ya Kiingereza hapa na pale. Hali hii ya kuchanganya ndimi hutokana na athari za ulumbilugha ambapo mtu anajipata akitumia lugha azijuazo katika mazungumzo. Mtu 1 pia anatumia lugha tatu katika usemi mmoja kama inavyobainika hapa chini:

2. Mtu 1: **Mzae (baba) alikuwa akiingia tu hivi kila kitu inachange (inabadilika) manze, anataka apewe nyake (nyama) na ugali na hata hataki**

**kujua itatoka wapi, akikosa anaanza kumpea beating (kichapo) tukiwa tumeketi tunawawatch (tazama) tu. Mathee (mama) hadi anafaint (zirai) na...**

Maneno, *mzae, manze* na *nyake* ni ya Sheng' na ambayo yametumiwa na Mtu 1 pamoja na maneno ya Kiswahili na Kiingereza katika usemi huu. Athari ya ulumbilugha inajitokeza zaidi Mtu 1 anapotumia maneno ya Kiingereza kwa kuchukua vitenzi vyake kisha kuviongezea viambishi awali vya Kiswahili kama inavyojitokeza katika maneno kama vile *inachange (ina-change)*, *tunawawatch (tunawa-watch)* na *anafaint (ana-faint)*. Washiriki wa mazungumzo haya wanachanganya ndimi kwa nia ya kurahisisha mawasiliano kwa kutumia maneno yatakayowawezesha kutumia muda mfupi katika mawasiliano. Mtindo wa kutumia lugha kwa kuchanganya mizizi ya maneno ya Kiingereza na kisha kuviongezea viambishi awali vya Kiswahili yanaonesha kuwa Mtu 1 anazifahamu lugha hizi mbili na ndio maana anaweza kuzichanganya katika mazungumzo yake. Mtu 4 pia anachanganya ndimi katika mazungumzo yake jambo linalodhahirisha athari za ulumbilugha kama inavyobainika katika mfano 3 ambapo anatumia vitenzi vya maneno ya Kiingereza huku akiongezea viambishi awali vya Kiswahili, mfano ni neno *tuliwatch (tuli-watch)* na vile vile kutumia maneno kamili ya Kiingereza kama vile *class* na *seven* kama ifuatavyo:

3. Mtu 4: **Weee unajua tuliwatch (tazama) akipiga tu mokoro (mama) tangu tukiwa watoi, na bado akaendelea tu, nilifika class (darasa) seven (saba) nikaamua kama mbaya, mbaya, akimchapa na mi nampiga hata na mwiko, hadi nilitoka kwake hivyo, sipendangi ujinga mimi.**

Katika mazungumzo tuliyoyashughulikia imebainika wazi kuwa *Chokoraa* ni wanaulumbilugha jambo ambalo wanalidhahirisha wanapozungumza. *Chokoraa* hawa wanachanganya ndimi kutokana na mazoea yao na ndio sababu washiriki wote wa mazungumzo haya wanatumia lugha kwa mtindo sawa. Mtindo wa kuchanganya ndimi katika mazungumzo yao. Tumeangazia *Chokoraa* wa jinsia ya kiume na kuonyesha kuwa wao hutumia lugha ya Kiswahili, Sheng' na Kiingereza katika mazungumzo yao. Tuligundua pia kuwa *Chokoraa* wa jinsia ya kike hutumia lugha hizi hizi katika mazungumzo yao kama inavyodhahirika katika diskosi ifuatayo tuliyorekodi mtaani Mathare katika eneo la Gitathuru:

4. Mtu 1: **Hao mauncle (wajomba) ni bad news (watu wabaya) haki.**  
Mtu 2: **Mimi hata sitakaangi kuwafikiria, naa.....**  
Mtu 3: **Kwani nyi nyote mlipata experience same (kupitia hali sawa)?**  
Mtu 2: **Maparo (wazazi) wote wakidedi (wakifa) ndio unajua mauncle (wajomba) na macuzo (binamu) ni wa aina gani. Ile kucheka mlikuwa mkicheka nao inakuwa machozi kila siku hadi unatamani kukunywa sumu ukufie huko but (ila) hata sijui mbona huikunywangi.**

Mtu 1: Eeh, mimi nilikunywa ratrat (*sumu*) na sikufa, haki walnikimbiza hosi (*hospitali*) na nilipopona nilitorokaanga na hata hakuna mtu alinitafuta.

Mtu 2: Huwezi tafutwa imagine.

Mtu 3: Wee huku upotee tu unatafutwa na mbogi (kundi) yako lakini huwezi tafutwa na marelatives (*aila*).

Mtu 2: Yaani watoto wao wanatreatiwa (*shughulikiwa*) poa halafu wewe huwezi buyiwa (*nunuliwa*) hata nguo ya mtush (*mtumba*) na kila saa ni kutukanwa matusi kubwa kubwa aaai, huko mmmh.

Mtu 1: Wengine wakimanga (*kula*) wewe unaambiwa uendee maji kwa kisima na saa hiyo line (*foleni*) ni kubwa ukirudi, keroma (*chakula*) imeisha unaosha tu vyombo na...

Mtu 3: Mi naye singeosha ka ni mimi wewe,

Mtu 1: Ukose uchapwe na ukose hata supper (*chajio*). Weeeh watu ni wanyama haki.

*Chokoraa* hawa wa jinsia ya kike wametumia Kiswahili, Sheng' na Kiingereza katika mazungumzo yao. Maneno ya Kiingereza katika diskosi hii ni kama vile: *bad news, experience, same, supper, but* na *line*. Sheng' pia imetumika hapa na mfano wa maneno ni kama vile *manga, keroma* na *mbogi*. *Chokoraa* hawa pia wamechanganya Kiswahili na Kiingereza kwa neno moja kwa kutumia vitenzi vya Kiingereza kisha kuongezea viambishi awali vya Kiswahili kama vile: *mauncle (ma-uncle)na marelatives (ma-relatives)*. *Chokoraa* hawa wa jinsia ya kike pia wamechanganya mizizi ya maneno ya Sheng' na kuongezea viambishi awali vya Kiswahili kama vile: *wakidedi (waki-dedi)* na *wakimanga (waki-manga)*. Tuligundua kuwa *Chokoraa* huchanganya ndimi zaidi wanapokuwa wakizungumza baina yao. Hii ni kwa sababu wanataka kujieleza ipasavyo kwa kutumia maneno kutoka kwa lugha tofauti ili kuleta athari inayokusudiwa kwa washiriki wa mazungumzo hayo kama inavyojitokeza katika usemi wa Mtu 2 anaposema kuwa “**Yaani watoto wao wanatreatiwa poa halafu wewe huwezi buyiwa hata nguo ya mtush na kila saa ni kutukanwa matusi kubwa kubwa...**” Mzungumzaji huyu anachanganya ndimi kwa kutumia lugha azijuazo za Kiswahili na Kiingereza. Vile vile anachanganya ndimi ili aweze kujieleza ipasavyo na hii ndio sababu anachanganya viambishi vya Kiswahili huku mizizi ikiwa ya Kiingereza. Mazungumzo ya kawaida pia hurusu matumizi ya lugha kwa kuzichanganya. Hii ni kwa sababu washiriki wa mazungumzo husika huwa na uhusiano wa karibu na hili ni jambo ambalo huwafanya kutumia lugha mbalimbali.

Tumegundua kuwa *Chokoraa* pia huchanganya ndimi katika mazungumzo yao kwa kujikita katika lugha za asili, Kiswahili, Sheng' na Kiingereza kama inavyojitokeza katika mazungumzo yafuatayo ambapo wametumia baadhi ya maneno kikuyu na lugha zingine:

5. Mtu 1: **Mokoro (mama) unapenda kutulenga (kutupuuza) siku hizi na...**

Mama: **Nyinyi hata mnasumbua watu, si mko wengi na siwezi pea kila mtu.**

Mtu 1: **Kwani una.....**

Mtu 2: **Mama ujue vile kumethoka (haribika) tunawategemea sana na...**

Mtu 3: **Wee aki tupee hiyo wera (kazi) haki.**

Mtu 2: **Kazi ndio tunataka tufanye haki.**

Mama: **Afadhalii wewe kijana huongei kama hawa, tuende na wewe uniokotee.**

Mtu 2: **Thanks (asante) mum haki.**

Hapa ni katika mtaa wa Mathare eneo la Gitathuru ambapo *Chokoraa* wanataka kazi kutoka kwa mama ambaye ni mwanakundi-nje. Kutohana na mazungumzo yao, tunabaini kuwa hawa ni watu walio na uhusiano wa karibu na ndio maana wanachanganya ndimi. Hili linadhihirika katika kipengele cha 1 ambapo Mtu 1 anasema kuwa, “**Mokoro unapenda kutulenga siku hizi na...**” Maneno haya yanashiria kuwa hawa ni watu ambao wamejuana kwa muda na ndio maana wanachanganya ndimi kwa kuwa uhusiano wao ni wa karibu.

Uhusiano wa wazungumzaji ni kichocheo cha uteuzi na utumizi wa lugha. Katika mazungumzo haya, washiriki wanachanganya ndimi kwa kujikita kwa Kiswahili, Kiingereza na Kikuyu. Uhusiano huu wa karibu ndio umewafanya kutumia lugha ya Kikuyu ambayo ni ya kiasili kama inavyojitokeza katika vipengele vifuatavyo:

6. Mtu 2: **Mama ujue vile kumethoka (haribika) tunawategemea sana na...**

Mtu 3: **Wee aki tupee hiyo wera (kazi) haki.**

Matumizi ya lugha ya kiasili yanadhihirisha kuwa *Chokoraa* na mfanyakishara wanafahamiana vyema. *Chokoraa* wametumia maneno ya Kikuyu kama vile *wera na thoka* katika mazungumzo ambayo Kiswahili kinatawala na kisha neno *thanks* la Kiingereza likachopekwa. Neno la Kikuyu, *mokoro* lina maana ya ajuza katika lugha husika ila hapa limepewa maana nyiningine ambayo mama.

Tumebaini pia kuwa *Chokoraa* huchanganya ndimi kwa nia ya kutumia maneno yaliyo na stara badala ya kutumia maneno ambayo hayafichi aibu kwa lugha waliyokuwa wakiitumia kama inavyobainika katika mazungumzo yafuatayo:

7. Mtu 1: **Aunty nisaidie tu.**

Mtafiti: **Aje mum?**

Mtu 1: **Aunty si unaelewa tu shida za wamama aki.**

**Mtu 2: Kwanza siku ya mashiroo (*hedhi*), unashindwa kusimama utafute kakitu.**

Mazungumzo haya yalikuwa kati ya mtafiti na *Chokoraa* wa kike katika eneo la Mashimoni. Lugha tatu zimetumika katika mazungumzo haya. Ipo lugha ya Kiingereza ambapo kuna neno *aunty*, Sheng' kuna neno *mashiroo*, na maneno hayo mengine ni ya Kiswahili. Tuligundua kuwa neno *mashiroo* la Sheng' limetumika kwa kuwa ni la stara ikilinganishwa na neno la Kiswahili. Kwa hali hii basi, *Chokoraa* wanatumia maneno ya lugha nyininge kwa nia ya kuficha aibu.

*Chokoraa* hawa wanazungumza kwa namna inayoibua hisia za huruma huku wakisema wazi kuwa walihitaji msaada ili kukidhi mahitaji yao kama inavyojitokeza kwa usemi huu wa Mtu 1, “**Aunty si unaelewa tu shida za wamama aki.**” *Chokoraa* huyu wa jinsia ya kike anazungumza na mtu wa jinsia sawia na yake. Ni kwa hali hii ambapo anaomba msaada kutoka kwa mwanamke mwenzake kwa kuwa wao hupitia hali sawa ingawa wapo katika makundi tofauti ya kijamii. Hili linajitokeza wazi kwa usemi wa Mtu 2 anaposema kuwa “**Kwanza siku ya mashiroo, unashindwa kusimama utafute kakitu.**” Mazungumzo ya aina hii hutokea kwa watu wa jinsia ya kike na hii ndio sababu *Chokoraa* hawa wanamweleza mtafiti ambaye ni wa jinsia ya kike pia.

**Uundaji wa Msamati Katika Lugha Vipindi**

Tumeonyesha namna ulumbilugha huwfanya *Chokoraa* kutumia lugha zaidi ya moja katika mazungumzo yao. Athari nyininge ya ulumbilugha inavyojitokeza katika mazungumzo ya *Chokoraa* wa Mathare ni kuchukua maneno ya lugha kama vile Kiswahili na Kiingereza na kisha kuyafanya kuwa ya Sheng' kwa kuyapa maana tofauti na maana yake asili kama inavyodhihirika katika mazungumzo yafuatayo:

8. Mtu 1: **Hii ni mbogi (kikundi) ya mtu saba bwana.**

Mtafiti: **Mtu saba tena!**

Mtu 1: **Inabidi tukae hivyo tuhustle (tutafute) kimoja.**

Mtu 2: **Wewe ulikuwa unatakaje ndugu?**

Mtu 1: **Huyu anakaa kukuwa liquid (kuwa na pesa) wacha atu.....**

Mtafiti: **Nadai kuzungumza na nyinyi kidogo tu.**

Mtu 1: **Hii ngware (asubuhi) yote hata breko (kiamsha kinywa) bado.**

Mazungumzo haya ni kati ya mtafiti aliyetaka kuwahoji *Chokoraa* wa Mathare katika eneo la Kosovo 3A majira ya saa tatu za asubuhi. *Chokoraa* hawa wanadhihirisha hali ambapo wanachukua maneno ya lugha nyininge na kuyapa maana tofauti na maana yake halisi katika Sheng' kama inavyobainika katika neno la Kiingereza *liquid* lenye maana ya kitu kioevu ilhali neno hili linatumika katika mazungumzo haya kumaanisha kuwa tajiri. Neno *breko* pia limefupishwa kutoka kwa neno la Kiingereza, *breakfast*. Ufupishaji wa maneno ya lugha fulani

---

umewawezesha kuunda msamiati mpya. Hali hii inaashiria uundaji wa maneno ya lugha vipindi kutoka kwa lugha zingine na hili ni jambo linaloashiria athari za ulumbilugha kwa *Chokoraa*.

*Chokoraa* pia huchukua baadhi ya maneno ya Kiswahili na kuyafanya ya Sheng' kwa kuyapa maana mpya. Hii ni njia nyingine ya kuunda msamiati mpya wa lugha vipindi ya Sheng' kama inavyojoitokeza katika mazungumzo yafuatayo:

9. **Mtu 1: Mtu nguyas (*wangu*) leo unakaa kuchoka sana.**

Mlinzi: **Vijana mnatakaje leo?**

Mtu 1: **Tunakugotea tu brathee (*tunakusalimia tu ndugu*).**

Mtu 2: **Sogi amejaas gas (*mlinzi amekasirika*).**

Mlinzi: **Nyinyi machokosh (*chokoraa*) mnakuja hapa kuongea vitu haieleweki.**

Mtu 2: **Aaah, usijali ni stori na mambogi (*ni suala la kuwa katika kundi moja*)**

Mlinzi: **Tokeni hapa au niwaitie polisi saa hii.**

Mtu 3: **Baas, cheza chini, cheza chini jooh (*tulia*)**

Katika mazungumzo haya, athari za ulumbilugha zinajitokeza kwa kuwa *Chokoraa* wametumia baadhi ya maneno ya Kiswahili na kuyapa maana mpya katika Sheng' hali ambayo inadhihirisha uundaji wa maneno katika lugha vipindi. Neno *gotea* ni la Kiswahili lenye maana ya kusinzia ilhali *Chokoraa* hawa wamelipa maana mpya ambayo ni kusalimia. Katika kipengele cha 4, Mtu 2 anasema kuwa '*sogi amejaas gas*' kwa maana kuwa mlinzi amekasirika. Katika diskosi hii, neno *sogi linatumiwa* kumrejelea mlinzi ilhali maana yake halisi katika Kiswahili ni mfuko utumiwao kubebaa mizigo kwa punda. Vile vile, Mtu 2 ametumia neno la Kiingereza *gas* kumaanisha hasira kinyume na maana yake halisi ambayo ni gesi. Maneno *cheza chini* ni ya Kiswahili na ambayo yanajisimamia kimaana, hivi kwamba neno cheza lina maana ya tikisika huku chini likiwa ni kinyume cha juu ilhali hapa maneno haya yametumika kwa maana ya kutulia jambo linaloashiria athari za ulumbilugha kwa *Chokoraa*.

#### **Ubadilishaji wa Mpangilio na Muundo wa Maneno**

*Chokoraa* wa Mathare pia wameathiriwa na ulumbilugha kiasi cha kuwafanya kubadilisha muundo wa maneno ya lugha zingine na kuwawezesha kuunda msamiati mpya wa Sheng' kama inavyobainika katika mazungumzo yafuatayo:

10. **Mtu 1: Umetokelezea wapi kwani wewe ?**

Mtu 2 : **Nilikuwa around.**

Mtu 1 : **Na vile tumekusakanya kila mahali.**

Mtu 2 : **Nilikuwa huko nyuma ya mloite (*choo*)**

Haya ni mazungumzo ya *Chokoraa*, mtaani Mathare katika eneo la Mashimoni. Neno *mloite* limeundwa kutoka kwa neno la Kiingereza, *toilet*. Muundo wa neno hili umebadilishwa kwa nia ya kuficha siri dhidi ya wanakundi-nje ila maana inabaki kuwa ile ile. Pia, uundaji wa msamiati mpya wa Sheng' unadhihirika hapa na hii inawezekana kutokana na athari za ulumbilugha. *Chokoraa* pia huweza kubadilisha sauti moja katika maneno ya Kiswahili kisha kuyapa maana kwa lugha ya Sheng' kama inavyobainika katika mazungumzo yafuatayo:

11. Mtu 1 : **Hao wasee (watu) wanatuchocha haki.**

Mtu 2 : **Kwanzaa huyo mzae (mzee) wa nyumba kumi.**

Mtu 1 : **Mi sitaki rada (maneno) yao.**

Mtu 2 : **Wale wameenda watatupeleka na rieng' (kutujuza).**

*Chokoraa* hawa wa Mathare wa eneo la Mashimoni wanadhihirisha athari za ulumbilugha katika mazungumzo yao. Wameunda msamiati wa Sheng' kwa kubadilisha sauti moja pekee katika maneno ya Kiswahili kisha maana inabaki kuwa ile ile au inabadilika. Neno *wasee* limeundwa kutoka kwa neno la Kiswahili, 'wazee'. Neno wazee lina maana ya watu walio na umri mkubwa au watu wa jinsia ya kiume na kisha *Chokoraa* wametoa sauti 'z' na badala yake kuweka sauti 's' na maana inabadilika na kuwa watu. Neno lingine ni *mzae* ambapo wametoa sauti 'e' (mzee) na kuweka sauti 'a' ila maana inabaki kuwa ile ile. Uundaji wa msamiati mpya wa lugha vipindi hutokana na ujuzi wa lugha zaidi moja kama tulivyobainisha katika mazungumzo tuliyoyaangazia na hili ni jambo ambalo linaashiria athari za ulumbilugha kwa *Chokoraa* wa mtaa wa Mathare.

### Hitimisho

Makala haya yameangazia athari za ulumbilugha katika mazungumzo ya *Chokoraa* katika maeneo mbalimbali ya mtaa wa Mathare, jijini Nairobi. Katika utafiti huu, imebainika kuwa ulumbilugha huwafanya kuchanganya ndimi katika mawasiliano yao ya kila siku. Tulibaini kuwa *Chokoraa* huchanganya ndimi kwa sababu ya kuwa na ujuzi wa lugha zaidi ya moja. Vile vile, *Chokoraa* huchanganya ndimi wanapozungumza wao kwa wao au na watu walio na uhusiano wa karibu nao. Uundaji wa msamiati mpya kila uchao hutokana na ari ya kutaka kupata maneno mapya kurejelea jambo au hali fulani na kwa njia hiyo wanaweza kuwatenga watu wa makundi mengine ya kijamii. Kwa hivyo, tunaweza kuhitimisha kwa kusema kuwa watu wenye sifa ya ulumbilugha hutumia lugha wazijuazo katika mazungumzo yao na pia huwa na uhuru wa kuteua lugha maalum ili waitumie katika muktadha mahsus.

### Marejeleo

- Abdulaziz, M. na Osinde, K. (1997). Sheng' and Engsh: Development of Mixed Codes among the Urban Youth in Kenya. *International Journal of the Sociology of Language* 125 (*Sociolinguistic Issues in Sub-Saharan Africa*) pp.4 5-63.
- Aronin, L. na Singleton, D. (2007). The Complexity of Multilingual Contact and Language Use in Times of Globalization. *International Journal of the Sociology of Language*, 2, 33-47.
- \_\_\_\_\_(2010). Affordances and The Diversity of Multilingualism. *International Journal of the Sociology of Language*, 205, 105-129.
- \_\_\_\_\_(2012). *Multilingualism*. Amsterdam: John Benjamins Publishers.
- Christopoulos, D. (2010). *Peer Esteem Snowballing: A Methodology for Expert Surveys*. Italy: IUSS Press.
- Flowers, R. B. (2010). *Street Kids: The Lives of Runaway and Throwaway Teens*. Mofarland: Jefferson NC.
- Gibson, J.J. (1977). *The Theory of Affordances: Perceiving, Acting and Knowing*. Hillsdale: Lawrence Erlbaum.
- \_\_\_\_\_(1986). *The Ecological Approach to Visual Perception*. Hillsdale: Lawrence Erlbaum.
- Githiora, C. (2002). Sheng: Peer Language, Swahili Dialect or Emerging Creole? *Journal of African Cultural Studies*, Vol. 15, No. 2, (Dec., 2002), pp. 159-181
- Habwe, J., Matei, A. na Nyonje, J. (2010). *Darubini ya Isimujamii kwa Shule na Vyuo*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Iribemwangi, P. na Mukhwana, A. (2011). *Isimujamii*. Nairobi: Focus Publishers Ltd.
- Kandagor, M. (2000). Uteuzi wa Istilahi Mionganii mwa Machokoraa nchini Kenya: Uchunguzi wa Mtaa wa Ngara, Nairobi. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Leech, G.N (1969). *A Linguistic Guide To English Poetry*. Edinburgh Gate: England: Pearson Education Limited.
- Lewis, S. (2012). *Homeless Children: Seventeen Moments in Soviet History*. Soviet: James Von Geldern.
- Massamba, D. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Muriira, M. P. (2016). A Complex Linguistic Code in Kenyan Linguistic Scene: A Case Study for Sheng. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi ambayo hajachapishwa.
- Ogechi, N. na Jwan, J. (2004). Bilingual Education for Street Children in Kenya: Evidence from Language Mixing. *Journal of Language and Learning* vol.2 no. 2 2004 ISSN 1740-4983
- Ray, S. (2017). A Street Child's Perspective: A Grounded Theory Study of How Street Children Experience and Cope With Grief. *The Qualitative Report*, 22(1), 291-308.

- Shorter, A. na Onyancha, E. (1999). *Street Children in Africa; A Nairobi Case Study*. Nairobi: Parlines Publications Press.
- Social Research Update 33: Accessing Hidden and Hard-to-Reach Populations. Sru.soc.survey.ac.uk. April 2017.
- Suda, C. (1997). Street Children in Nairobi and the African Cultural Ideology of Kin-based Support System: Change and Challenge. *Child Abuse Review* Vol. 6.